

## Taratibu za Uundaji wa Maneno Ambatani ya Lugha ya Kiswahili

na

Hashim Juma na Nashukuru Sanga

*Ikisiri*

*Maneno ni vipashio muhimu katika lugha ya Kiswahili. Umuhimu wake unatokana na kuwa maneno ni vipashio huru ambavyo hudokeza maana. Kadhalika, maneno hayo ambayo hudokeza maana yamekuwa yakiundwa kutokana na michakato mbalimbali ya kimofolojia ya uundaji maneno, mionganini mwa michakato hiyo ni uambatani. Hata hivyo, miundo ambatani huwa na taratibu maalumu ya utokeajji wake katika lugha ya Kiswahili. Hivyo basi, makala haya yamekusudia kuonesha taratibu maalumu za kuzingatia kwenye miundo ambatani katika lugha ya Kiswahili.*

### 1.0 Utangulizi

Dhana ya mwambatano imefasiliwa na wataalamu kadhaa. Mionganini mwa wataalamu hao ni Katamba (1993) ambaye anaeleza kuwa mwambatano ni utaratibu wa kuunda maneno kwa kuunganisha angalau maneno mawili au zaidi. Aidha, Massamba (2009) anaeleza kuwa mwambatano ni hali ya vipashio huru viwili au zaidi kukaa pamoja ili kuwakilisha dhana moja mpya. Tukiitazama fasili ya Massamba (k.h.j) tunabaini kuwa ina mapungufu, kwani sio lazima neno ambatani liundwe na vipashio huru viwili kwani kuna baadhi ya maneno ambatani huundwa na kipashio huru pamoja na kipashio kisicho huru. Mfano **kwa nini, kwa sababu**. Katika mifano hiyo, neno ‘kwa’ halina hadhi ya kipashio huru kwa kuwa haliwezi kusimama peke yake na kutoa maana. Vilevile, dhima yake hubadilika badilika kutegemeana na nafasi na uamilifu wake katika sentensi.

Baada ya kuzipitia fasili za wataalamu kuhusu dhana ya mwambatano, tumehitimisha kwa kusema kwamba, mwambatano ni mchakato wa kimofosintaksia ambapo maneno mawili au zaidi huambatanishwa kwa utaratibu maalumu ili kuunda neno jipya. Mchakato huu ni wa kimofosintaksia kwa sababu huusisha mofolojia ambayo inajihusisha na uundaji wa maneno na sintaksia kwa kuwa hujihusisha na mahusiano ya maneno hayo katika kuunda neno jipya.

## **2.0 Uhusiano wa Vjenzi vya Maneno Ambatani**

Uhusiano wa vjenzi vya maneno ambatani huweza kuainishwa katika aina tatu ambazo ni mahusiano ambatani yumishi, mahusiano ambatani tegemezi na mahusiano ambatani huru (Gichuru, 2010). Kuhusu mahusiano ambatani yumishi ni aina ya uhusiano ambapo neno lisilokuu hutoa maelezo zaidi kuhusu neno kuu. Tazama mfano wa 1 kwa ufanuzi zaidi.

Mfano wa 1

- i. Kiambishi **awali**
- ii. Waziri **mkuu**
- iii. Raisi **mteule**
- iv. Pembe **kali**

Katika mfano wa 1 hapo juu, maneno yaliyokozwa yanafanya kazi kama vivumishi yaani yanatoa maelezo zaidi juu ya maneno yaliyoambatana nayo. Hivyo, uhusiano huu huitwa uhusiano yumishi

Kwa upande wa maneno yanayoambatana kuunda neno ambatani huwa na hadhi sawa. Aidha, maneno hayo aghalabu huwa ni ya kategoria moja. Tazama mfano 2 kwa ufanuzi zaidi.

Mfano 2

- i. changamoto
- ii. kiberitingoma
- iii. jamiilugha

Katika mfano 2, vjenzi vya neno ambatani vina hadhi sawa na maneno. Hivyo, uhusiano wa namna hiyo wa vjenzi huitwa uhusiano ambatani huru.

Uhusiano mwingine ni ule wa mahusiano ambatani tegemezi. Katika uhusiano huu kijenzi ambacho ni neno kuu hutegemeana na kijenzi ambacho si neno kuu katika kuunda neno ambatani. Aidha, hali hii hutokea pale ambapo kijenzi kimoja ni kitenzi au neno lililoundwa kutokana na kitenzi. Tazama mfano 3 kwa ufanuzi zaidi.

- i. Mfanyabiashara
- ii. Chemshabongo
- iii. Mpigambizi

Katika mfano 3 maneno yaliyokozwa yanafanya kazi kama yambwa kwa kuwa maneno hayo huelekezewa tendo linalofanyika.

## **2.0 Miundo ya Maneno Ambatani**

Maneno ambatani huwa na miundo tofautitofauti kutegemeana na maneno yanayoiunda. Aidha, miundo hii huongozwa na kanuni ya miundo virai ya lugha husika (Katamba, 1993; Buberwa, 2018). Maelezo haya yana maana kuwa, maneno yanayounda neno ambatani yanapaswa kupangiliwa kwa utaratibu maalumu. Kama kanuni ya miundo virai haitazingatiwa tunaweza kupata maumbo yasiyokubalika katika lugha husika.

Aidha, Lieber (2010) anaeleza kuwa maneno ambatani huweza kuainishwa katika makundi mbalimbali kwa kuzingatia muundo wake yaani idadi ya vijenzi vinavyounda neno ambatani. Kulingana na kigezo hiki tunapata aina kuu mbili za maneno ambatani ambazo ni maneno ambatani sahili na maneno ambatani changamani. Aidha, kuhusu maneno ambatani sahili huundwa na maneno mawili, mfano isimujamii, waziri mkuu, patapotea. Kadhalika, maneno ambatani changamani huundwa na maneno zaidi ya mawili mathalani kiimbo-toni msingi, sarufi miundo-virai, pembe-tatu pacha.

Katika lugha ya Kiswahili maneno ambatani huwa na miundo tofauti tofauti kutegemeana neno linalotakiwa kuundwa. Kwa kuzingatia lugha ya Kiswahili tumedhihirisha kauli isemayo kwamba, “Miundo ambatani katika lugha ya Kiswahili huzingatia taratibu maalumu” na taratibu hizo tumeweza kuziangalia kupitia kigezo cha kisintaksia na kisemantiki. Hebu tutazame hizo taratibu zinavyojionesha katika miundo ambatani.

Mosi, neno lenye ujazo mkubwa kisemantiki ndilo huanza, Halliday (1985) anaeleza kuwa, ujazo wa kimaana ni hali ya neno kuweza kujitosheleza kimaana au kutojitosheleza kimaana. Halliday (k.h.j) anaendelea kueleza kuwa kategoria za kileksika kama vile nomino, vitenzi, vivumishi na vielezi huwa na ujazo mkubwa kimaana kuliko kategoria za kisarufi. Hata hivyo, katika kategoria za kileksika nomino ndizo huwa na ujazo mkubwa wa kimaana kuliko kategoria nyingine za kileksika. Kutokana na maelezo hayo, utaratibu huu huwa unazingatiwa katika miundo ambatani. Tazama mfano 4 kwa ufanuzi zaidi.

#### Mfano 4

- i. **Mwalimumkuu**
- ii. **Mwanaharamu**
- iii. **Wazirimkuu**
- iv. **Kiambishitamati**

Katika mfano (i-iv) maneno yaliyokozwa yapo katika kategoria ya nomino na vilevile yana ujazo mkubwa wa kisemantiki. Kadhalika, maneno hayo yapo katika miundo ambatani sahili. Katika data yetu (i-iv) maneno yenyе ujazo mkubwa wa kisemantiki yanaanza kisha kufuatiwa na kivumishi ambapo vivumishi vina ujazo usio mkubwa ukilinganisha na nomino. Hivyo, tunagundua kuwa katika miundo ambatani utaratibu wa kuzingatia ujazo wa kisemantiki huzingatiwa wakati wa kuunda maneno ambatani. Hata hivyo, si mara zote maneno yenyе ujazo mkubwa wa kisemantiki kuanza mwanzoni kwani kuna baadhi ya maneno katika miundo ambatani huanza na neno lenye ujazo mdogo wa kisemantiki mathalani maneno kama kwa sababu, kwa mkapa, kwa nini.

Pili, utaratibu maalumu mwingine unaozingatiwa katika miundo ambatani ni neno ambalo ni hipanimu huwa linatangulia na kufuatiwa na hiponimu, Resani (2014) anaeleza kuwa hipanimu ni neno lenye maana kubwa au neno kuu ilhali hiponimu ni maneno yenyе maana ndogo. Kulingana na maelezo hayo, tumebaini kuwa hipanimu na hiponimu zina uhusiano wa karibu mathalani tunda ni hipanimu lakini embe, nanasi, chungwa hizi ni hiponimu. Aidha, katika miundo ya maneno ambatani utaratibu wa hipanimu kutangulia na kufatiwa na hiponimu unazingatiwa ili kuunda maneno ambatani. Hebu tazama mfano wa 5 kwa ufanuzi zaidi.

## Mfano wa 5

- i. **Kiambishiawali**
- ii. **Batamzinga**
- iii. **Sarufimaumbo**
- iv. **Isimujamii**
- v. **Pembe-tatu Pacha**

Katika mfano (i-v) maneno yaliyokozwa ni hipanimu ambayo kimsingi ndiyo yaliyobeba dhana pana. Mfano hipanimu kiambishi hujumuisha kiambishi awali, kiambishi tangulizi na kiambishi tamati. Vilevile, hipanimu bata hujumuisha batamaji, batamzinga, pia hipanimu sarufi hujumuisha sarufi miundo, sarufi maana na hipanimu isimu hujumuisha isimujamii, isimu historia, isimulinganishi na pembe huweza kujumisha pembe kali, pembe mraba, pembe tatu. Hivyo basi, maneno katika data yetu (i-v) yameundwa na hipanimu na hiponimu. Licha ya kuwa na mfuatano wa hipanimu na hiponimu katika kuunda maneno ambatani, ipo miundo ambatani ambayo kimsingi haiongozwi na utaratibu huu mathalani maneno kama kiberitingoma, pepopunda. Katika maneno kama kiberitingoma na pepopunda hakuna hipanimu yaani hakuna neno kuu ambalo linajumuisha neno jingine ndani yake.

Tatu, utaratibu mwingine ambao unazingatiwa katika miundo ambatani ni kipashio cha muhimu ndicho huanza katika kuunda neno ambatani. Katika kuelezea hoja tumejikita katika kipengele cha maana dhamira. Resani (2014) anaeleza kuwa hii ni maana ambayo huwasilishwa kwa kutegemea namna msemaji au mwandishi alivyopangilia ujumbe kimfuatano na kimsisistizo. Aidha, Resani (k.h.j) anaendelea kueleza kuwa, kinachotokea kwanza ndicho muhimu. Kutokana na maelezo hayo tunabaini kuwa, neno lianzalo katika miundo ambatani ndilo la muhimu, pia neno hilo huwa la msingi katika muktadha fulani ndio maana huwa la kwanza na kufuatiwa na maneno mengine. Hebu tazama mfano wa 6 kwa ufanuzi zaidi.

## Mfano wa 6

- i. **Isimujamii**
- ii. **Fonolojia** vipande-sauti huru
- iii. **Sarufi** geuza-maumbo

Katika mfano wa (i-iii) maneno yaliyokozwa ni maneno ya muhimu kwani ndio yameanza katika kuunda neno ambatani. Aidha, katika muktadha wa lugha neno isimu, fonolojia na sarufi ndio maneno ya msingi. Pia, utaratibu huu usipozingatiwa tunaweza kupata maneno ambatani yasiyokubalika. Hata hivyo, ipo miundo ambatani ambayo neno linaloanza sio la msingi mathalani maneno kama ‘kiberitingoma’ na ‘mjombakaka. Maneno kama kiberiti ngoma na mjombakaka yanashindwa kutusaidia kwamba, ni katika miktadha ipi neno kiberiti ni muhimu na neno mjomba ni muhimu katika miktadha ipi. Hivyo, maneno kama haya yanashindwa kuingia kwenye kigezo kisemacho neno la msingi ndilo huanza katika miundo ambatani.

Nne, taratibu nyingine inayozingatiwa katika miundo ambatani uundaji ni kwamba, nomino hisivu sharti ianze na kufuatiwa na nomino isiyo hizivu. Kimsingi, katika lugha ya Kiswahili nomino hisivu huwakilisha binadamu na wanyama ilhali nomino isiyo hisivu huwakilisha vitu kama vile mawe, miti. Katika uundaji wa maneno ambatani nomino hisivu huanza kisha kufuatiwa na nomino isiyo hisivu. Hebu tutazame mfano 7 kwa ufanuzi zaidi.

#### Mfano 7

- i. **Mpigapicha**
- ii. **Mjamzito**
- iii. **Mwanaharamu**
- iv. **Waziri** mkuu

Katika mfano (i-iv) maneno yaliyokozwa ni nomino hisivu. Nomino hizo zimeanza kisha kufuatiwa na nomino zisizo hisivu. Utaratibu huu umezingatiwa katika kupata maneno hayo ambatani. Hata hivyo, utaratibu huu unakumbana na changamoto kadha kama vile ipo miundo ambatani ambayo kimsingi yanaundwa na nomino hisivu mbili mathalani askaripolisi, mwanahamisi, patapotea. Hivyo, utaratibu wa nomino hisivu kuanza unashindwa kutumika katika maneno hayo.

### **4.0 Hitimisho**

Makala haya yamejadili dhana ya uambatani, vijenzi vya maneno ambatani pamoja na taratibu maalamu ambazo miundo ambatani huzingatia. Vilevile, makala haya yamebaini kuwa mpangilio wa vijenzi katika miundo ambatani haitokei hivi hivi bali huongozwa na taratibu za kisintaksia na kisemantiki. Aidha, taratibu hizo zimebainishwa katika kipengele cha (3.0) katika makala haya.

Hivyo, mwanamofolojia hana budi kuzifahamu taratibu hizo pindi anapoyashughulikia maneno ambatani.

### **Marejleo**

- Buberwa, A. (2018) “Uchunguzi Linganishi wa Kirai na Neno Ambatani katika Kiswahili”. Katika, Mwanga wa Lugha. Dar es salaam: Moi University Press.
- Gichuru, T.M (2010) “Uchanganuzi wa Nomino Ambatani za Kiswahili: Mtazamo wa Mofolojia Leksika”. Tasnifu ya Umahiri (haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Kenyatta, Nairobi.
- Halliday, M.A (1985) *Lexical Density and Readability*. Dealan University.
- Katamba, F (1993) *Morphology*. New York: Palgrave.
- Lieber, R (2010) *Introducing Morphology*. New Hampshire. New York: Cambridge University Press.
- Massamba, D.P.B (2009) *Kamusi ya Isimu na Falsafa ya Lugha*. Dar es Salaam: TUKI.
- Resani, M (2014). *Semantiki na Pragmatiki ya Kiswahili*. Dodoma. Karljamer Publishers.